

MKATABA WA KUKODISHA SHAMBA

MKATABA HUU umefanyika leo tarehe 01 Mwezi 02 2020

BAINA YA

AMH ENTERPRISES LTD wa Sanduku la Posta 708 Mwanza (ambaye katika mkataba huu ataitwa "**MPANGISHAJI**") kwa upande mmoja,

NA

CANUCK COMPANY LIMITED wa Sanduku la Posta 7323, Dar es Salaam (ambaye katika mkataba huu ataitwa ("**MPANGAJI**") kwa upande mwingine,

KWA KUWA MPANGISHAJI ni mmiliki wa shamba katika kitongoji cha **MANGUHU'NGWA** katika kijiji cha **MANGUHUN'NGWA**, wilaya ya **MSALALA**, Mkoa wa **SHINYANGA** ambaye anahitaji kukodisha shamba hilo lenye ukubwa wa hekari 16 kwa mpangaji tajwa hapo juu kwa ajili ya kufanya shughuli za uchimbaji wa madini kwenye leseni yake ya madini.

NA KWA KUWA Mpangaji yuko tayari kukodi/kupanga shamba lililotajwa hapo juu katika mkataba huu kwa ajili ya kufanya shughuli za uchimbaji wa madini katika leseni yake ya madini.

HIVYO PANDE ZOTE MBILI ZIMEKUBALIANA KAMA IFUATAVYO: -

1. **KWAMBA MPANGAJI** atalipa kiasi cha shilingi milioni moja tu (**1,000,000/=**) tu kila mwaka kama ada ya kukodi eneo tajwa
2. **KWAMBA** kiasi cha pesa katika aya ya kwanza kwaajili ya mwaka 2020 kitakuwa kimelempwa wakati wa kusainiwa kwa mkataba huu.
3. **KWAMBA** mkataba huu utadumu kwa muda wa miaka mitatu tu (3)
4. **KWAMBA MKATABA** huu unatawaliwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa yeyote atakayekiuka Masharti ya Mkataba huu, hatua za Kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa upande ule utakaodhurika.

KAMA USHAHIDI wa makubaliano haya mkataba huu umetiwa saini pande zote mbili kwa namna na tarehe inavyoonyesha hapa chini

UMESAINIWA hapa **MWANZA** na MUZAFFARALY NATHU **Kwa niaba ya AMH ENTERPRISES LIMITED** ambaye Namfahamu/Ametambulishwa Kwangu nana ambaye namfahamu binafsi Leo tarehe 01 mwezi 02 2020

[Signature]
.....
MPANGISHAJI

MBELE YANGU:

JINA: ANDREW I. LUHIGO
ANWANI: S.L.P. 4026, Mwanza
CHEO: MAKIU
SAHIHI: [Signature]



UMESAINIWA hapa **MWANZA** na CHAD BEATTIE
Kwa niaba ya **CANUCK COMPANY LIMITED**
ambaye Namfahamu /Ametambulishwa kwangu
na na ambaye namfahamu
binafsi leotarehe..01...mwezi...02... 2020


MPANGAJI

MBELE YANGU:

JINA: ANDREW I LUHIGO
ANWANI: S.L.P. 4026, MWAANZA
CHEO: WAZILI
SAHIHI: 

